# Zab 145-Nitamuimbia zaburi

## 23è DTO-B

Toni Iragi K




1. Bwana anashika uaminifu hata **milele,**
anawarudishia haki waliozu**lumiwa.**
Bwana anawapa wenye nja**a mkate,**
Bwana anawafungua **wafungwa.**

2. Bwana anafumbua macho ya **vipofu,**
Bwana anawainua walio**inama.**
Bwana anawapenda wa**tu wema,**
Bwana anawalinda **wageni.**

3. Anawatunza yatima **na mjane,**
ila anapotosha njia ya **waovu.**
Bwana atatawala **milele,**
Mungu wako, ee Sioni, kizazi kwa **kizazi.**